NIPASHE
ELIMU
Alhamisi ■ Novemba 25, 2010



Na Happy
SEVERINE, NEWALA



# Ulevi unapokuwa chanzo cha kuharibu taaluma ya walimu Wilayani Newala

Kosa gani tulilomkosea Muumba hata atufanye hivi?.....Ndivyo wanavyoeleza walimu wa shule ya Msingi Mkoma 1 iliyoko umbali wa kilometa zaidi ya 20 kutoka Newala mjini.

Haya yalikuwa ni baadhi ya malalamiko ya mwalimu Mtongwela Hamis, Lamimu Ibrahimu na Msafiri Seleman niliowakuta wakiwa wamekaa ofisini kwao katika shule hiyo ya Mkoma 1 huku wakionyesha kutokuwa na furaha.

Niliingia ofisini hapo na kuanza kuwasalimia...na baada ya salamu nilimuuliza mmoja kati kisa hasa cha kuonekana kwenye hali hiyo na nini hasa kinasaabisha hadi waseme hivyo.

Wao walikuwa wakijadiliana juu ya hali ambayo imewakumba baadhi ya walimu wenzao ambapo kutokana na mazingira wanayofanyia kazi wamejikuta wakijihusisha zaidi na ulevi kuliko kujikita kwenye kazi.

Selemani anasema kwa upande wake anadhani hali hiyo imekuwa ikichangiwa na kufanya kazi katika mazingira ambayo ni duni kiasi cha kuwakatisha tamaa.

Mwalimu huyo hakusita kunieleza kuwa wanahuzunika sana kwani maisha ya walimu yamezungukwa na matatizo makubwa yakiongozwa na suala zima la mazingira duni ya nyumba wanazoishi , nyingi zake zikiwa ni zile zilizojengwa kwa udongo tena za kupanga kwa wenyeji eneo lililoko mbali na shule.



Mwalimu Hashim Chihenge wa shule ya Msingi Mwangaza akiwa amesimama nje ya nyumba yake.N yumba nyingi wanaozoishi walimu haziko kwenye mazingira mazuri, jambo analosema linafanya wengine wawe walevi.

na wawili wapo tume ya utumishi ya walimu.

Matatizo mengine ni mazingira yasiyovutia Tatizo hilo limesababisha walimu kukimbia wilaya hiyo. Kwa mfano, kati ya nyumba 1,155 zinazohitajika kwa walimu, zilizopo ni 233 na hivyo kuna upungufu wa nyumba 922.

Hali hiyo inafanya walimu kuishi mbali na maeneo yao ya kazi.

Na Kuhusu uwajibikaji wa wazazi kwa wanafunzi, ilibainika kuwa wazazi wengi hawana uangalifu wa karibu kwa watoto wao hasa wa kike na badala yake huachiwa walimu peke yao.

Mkazi mmoja wa kijiji cha Mkunya ,Isumai Juma (45) alisema kutokuwepo kwa walimu wa kutosha kunasababisha watoto kushinda nje ya madarasa wakicheza, na wakati mwingine hata kuwafanya wanafunzi hao kutopenda shule.

Pia, walimu wachache waliopo wilayani humo wanalazimika kufundisha vipindi vingi kwa siku hali inayowafanya kushindwa kufikia viwango stahili cha ufundishaji.

Mary Sambi ni mwalimu mkuu katika shule ya msingi Tawala na anasema kuwa licha ya kukabiliwa na jukumu la kiutawala, pia analazimika kufundisha kwa muda mrefu zaidi kutokana na uchache wa walimu shuleni hapo.

"Nimejipangia kufundisha darasa la kwanza na la pili wakati wa asubuhi na mchana na kuwa na darasa la saba na sita....Nakosa muda wa kupumzika, lakini hata ule uwezo wa kufundisha kwa kiwango na maelekezo ya kanuni za maandalizi ya vipindi kwa hakika huwa ni vigumu kuyafikia."

Nilitaka kujua kwa undani mazingira mabovu ya walimu yanasababishashe kuwepo kwa tatizo la ulevi wa kupindukia kwa baadhi ya walimu wilayani hapo.

Mwalimu , Ibrahim anasema kuwa kutokana na mazingira kuwa si mazuri kiasi kwamba hata wamalizapo muda wa kufundisha hawana hamu ya kurudi nyumbani kupumzika kwani nyumba hizo ni kero kwao hivyo baadhi wanaamua kwenda vilabu vya pombe za kienyeji na kunywa kupoteza mawazo.

Hata hivyo wananchi bila kujua chanzo cha ulevi wa kupindukia kwa walimu wilayani hapo , wameonekana kukerwa na tabia ya baadhi ya walimu kulewa kupindukia, hali inayowafanya kushindwa kufanya kazi zao kama kanuni na masharti ya ajira zao zinavyotaka.

Mwalimu Mkuu Msaidizi wa shule ya Msingi Mkomal Lamimu Ibrahim Nanyenje , anasema kuwa kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi juu ya walimu kulewa pombe , bila ya wananchi hao kuchunguza nini hasa sababu ya walimu hao kunywa pombe.

"Mimi nawaomba wananchi waache kuwamwagia walimu lawama bila kufanya uchunguzi wa hizo lawama ....wajue nini hasa kinawasababishia hadi walimu hao kulewa.

"Hebu angalia nyumba tunazoishi hazina tofauti hata kidogo na wanakijiji...vyoo vyetu vya nyasi ,nyumba mbavu za mbwa, majiko yetu sawa na viota vya ndege....hivi haya maisha hamyaoni kuwa ni matokeo ya huo ulevi,' anasema Mwl Nanyenje.



Mke wa Mwalimu , Mtongwela Hamis wa shule ya Msingi Mkoma 1 Newala akionyesha jinsi ukuta wa nyumba waishio ulivyobomoka na kutapakaa nyufa.

Afisa Elimu wa Wilaya ya Newala Antony Alphonce alisema walimu wapatao 117 wilayani humu, walibainika kuwa ni walevi wa kupindukia katika kampeni ya wiki ya elimu duniani iliyofanyika April mwaka huu, hivyo kuwafanya walimu hao hushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo, na kuifanya wilaya hiyo kuwa chini kitaaluma.

Alphonce anasema wilaya ya Newala inakabiliwa na tatizo la walimu kulewa, ila kwa sasa idadi ya walimu hao walevi inapungua siku hadi siku kutokana na jitihada wanazozifanya za kuwachukulia walimu hao hatua za kinidhamu .

"Katika kuipunguza idadi hiyo ya walimu 117 walevi, tulianza kuwakabidhi walimu hao kwa CWT kwa hatua za awali...baadaye tutakaa nao na kuona nini kifanyike... ila nashukuru kwani idadi hiyo inapungua ingawa siwezi kukwambia imepungua kwa kiasi gani."

Kwani anasema suala la mtu kuacha pombe ni vigumu kwa mafanikio yake kuonekana mara moja na hata kama wanakunywa basi watakuwa wanafanya hiyo kwa kujiheshimu.

Hata hivyo Afisa huyo alisema kumekuwepo na malalamiko mengi kutoka kwa wazazi pindi wawaonapo walimu hao wakilewa mno hali inayowafanya kushindwa kuhudhuria vipindi vyao kikamilifu.

Alphonce y alisema tayari wamekwisha weka mkakati wa kukabiliana na tatizo hilo , ikiwa ni pamoja na wananchi kuacha tabia ya kuwauzia walimu pombe wakati wa masomo.

Hata hivyo alishauri pia kamati za shule zishirikiane na serikali za vijiji ambazo zilipewa jukumu la kudhibiti walimu walevi ili kuhakikisha tatizo hilo linakwishawwilayani hapo.

Hata hivyo Afisa Elimu wa Mkoa Hipson Kipenya alisema kuwa licha ya kuweo kwa walimu walevi ambao wanashindwa kuwajibika ipasavyo , kuna upungufu pia wa walimu wilayani humo .

Akitolea ufafanuzi wa shaua hilo Kipenya alisema kuwa ,wilaya ya Newala yenye vijiji 155, ina shule za msingi 117 na walimu wanaofundisha madarasani ni 840, huku 12 wakiwa ofisi ya wilaya, 21 ni waratibu elimu kata

vigumu kuyafikia."

Anasema licha ya kuwa na vipindi vini kiasi hicho bado analazimika kufanya majukumu wengie ya kiutawala kama mwalimu mkuu.

Akitoa ufafanuzi juu ya upungufu wa walimu Afisa Elimu Wilaya ya Newala alisema kwa ni kweli kuna upungufu, lakini kwa sasa tatizo ni mgawanyo wa walimu waliopo, kwani ukiangalia ikama na kanuni za wanafunzi 40 kwa mwalimu mmoja, upungufu unaonekana ni mdogo.

"Nataka niseme hivi...pale mjini Newala shule zote zina walimu wa kutosha na pengine ingewezekana kuwapunguza na kuwapeleka katika shule nyingine vijijini...lakini kila mwalimu pale mijini ana sababu zinazimfanya kuwepo pale..., wengine ni wagonjwa wa kudumu na wanalazimika kuwa karibu na hospitali ya wilaya. Wengine ni wake za watumishi, huwezi kuwapeleka mbali na waume zao," anasema Alphonce

Sula la ulevi linapokuwa ni tatizo kwenye jamii katika njanja yoyote ile mara nyingi imekuwa ni chanzo kikubwa cha kudidimia kwa maendeleo. MwMhadhiri kutoka Chuo cha ustawi wa Jamii kilichoko Dar es Salama, Hawa Madiwa anasema ingawa walimu wa Newala wanaeleza kuwa kinachowachangia wajiingize kwenye ulevi ni mazinigira duni ya nyumba wanazoishi anasema kuna weza kuwa na sababu nyingine zilizojificha.

"Wako watu ambao wanaamua kuwa walevi kutokana na msongo wa mawazo wakati wengine kwao hiyo ni tabia na kutokujali wajibu wao,' anasema Modiwa.

Anasema pia wakati mwingine uhusiano mbaya kwenye ndoa nao unaweza kuchangia hali hiyo na mara nyingi kuifanya familia iweze hata kusambaratika.

Hivyo anasema kuwa licha ya walimu kama hao kuchukuliwa hatua mbali mbali za kinidhamu kuna umuhimu wa kufanyiwa ushauri nasaha huku wahusika wakijua kwa undani hasa nini kinachangia idadi kubwa hivyo ya walimu huko Newala kujiingiza kwenye ulevi wa kupidukia.

# Uhaba wa walimu wakwamisha sekondari za kata Mtwara

ONGEZEKO la shule za sekondari za umma ( za kata) linaungwa mkono na watu karibu wote wanaopenda kuona maendeleo ya elimu yanawafikia watu wengi zaidi. Hata hivyo, mazingira duni ya shule hizo bado ni kikwazo kikubwa cha kufikia azma iliyokusudiwa. Makala haya yaeleza.

UKIANGALIA mazingira duni ya mwalimu vijijini, mara nyingi waweza kujiuliza swali lifuatalo: Je, ukimwona mtu anakufa kwa kiu ya maji na wewe una tone moja tu la maji, utampa hilo tone au utafanya nini?

Yawezekana likakosekana jibu sahihi, ila katika sera za huduma kwa jamii ikiwemo suala la utoaji wa elimu, ni kwamba kama serikali haina uwezo wa kugharamia utoaji wa elimu inayotakiwa au huduma yoyote ya kijamii ni muhimu kuchukulia kwa umakini mkubwa.

Mwenendo wa shule za umma maarufu kwa jina la shule za kata, siyo wa kuridhisha sana licha ya kuwa lengo lake ni zuri.

Hivi karibuni, vyombo vya habari kadhaa viliripoti taarifa ya kusikitisha kuhusu shule moja ya kata ambayo wanafunzi wake walilazimika kufanya mitihani wakiwa wamekaa chini na baadhi yao wakiwa chini ya mwembe.

Taarifa hii si ya kufurahisha hata kidogo hasa ikizingatiwa kuwa mara kwa mara kelele zimekuwa zikipigwa kuhusu kero mbalimbali zilizopo katika shule hizo. Ni mazingira hayo ndiyo yanayochangia kusababisha wanafunzi wengi kufeli katika shule hizo kama ilivyoshuhudia katika mtihani wa kidato cha nne mwaka 2010.

Wanafunzi wengi waliofeli wamekuwa mzigo kwa taifa, ambapo elimu waliyoipata sio tu haikuwawezesha kuingia kidato cha tano, lakini pia itawaweka katika mazingira sio mazuri sana ya kukabiliana na changamoto za maisha katika maeneo wanayoishi.

Mwanafunzi mmoja, Shabani Juma wa shule ya sekondari ya Chuno iliyopo mjini Mtwara , anasema kuwa shule za kata ni kama haziwasaidii sana kuwapa elimu bora kwa sababu raslimali walimu na vifaa havitoshelezi na ndio sababu ya wanafunzi wengi kuendelea kufeli.

" Wazo la serikali kuanzisha shule za kata kwa lengo la kuhakikisha kila mwanafunzi anapata huduma ya elimu jirani na anakotoka halikuwa baya....lakini shule hizo bado zina mapungufu makubwa mno...Hazina walimu wa kutosha, vitabu, na maabara...na kwa hali halisi ninaweza kusema kuwa shule za kata zimeanzishwa kwa shinikizo la kisiasa," alisema.

Juma Rashidi ni mwanafunzi wa kidato cha nne katika shule ya Sekondari Sino, anasema kuwa uanzishwaji wa shule hizo ni kama hakukufanyika maandalizi ya kutisha na mipango madhubuti ya kuratibu ongezeko la uandikishwaji wa wanafunzi wa kidato cha kwanza kufuatia ongezeko la wanafunzi wa darasa la saba waliotokana na mafanikio ya awamu ya kwanza ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM)

Alisema kuwa, inawezekana Serikali haikuwa makini sana katika kuhakikisha kuwa shule hizo zinashamiri kila kona ya nchi, bila kujali mahitaji na mategemeo ya wanafunzi. Matokeo yake ni kuwepo kwa upungufu mkubwa wa mahitaji muhimu katika utoaji na upatikanaji wa elimu.

Aidha Afisa Elimu wa Mkoa wa Mtwara ,Hipson Kipenya, alisema shule hizo za kata zikisimamiwa vyema, zinaweza kutoa elimu bora kwa gharama kidogo. Kwa sasa, shule hizo licha ya kulenga kuwasaidia wanyonge, zimeshindwa kurandana na matarajio ya wananchi wengi hasa wale wa vijijini.



Afisa elimu wa Mkoa wa Mtwara, Hipson Kipenya

Mwajuma Mohammed ni mwanafunzi wa shule ya Sekondari ya kata iitwayo Sino anasema kuwa kama wazazi wa wanafunzi hao wasingekuwa makini kufuatilia maendeleo ya watoto wao, shule hizo ni kama zimekuwa mwiba mkali kwao ambapo wanajikuta wanavumulia watoto wao kusoma katika shule hizo kwa sababu hawana shule mbadala kwa ajili ya watoto wao ili wapate elimu bora.

" Wazazi wenzangu walipohamasishwa kujitolea kujenga shule hizo, serikali nayo ingetekeleza wajibu wake kwa kuhakikisha kuwa inazipatia vifaa, walimu na kuboresha mazingira ya kujifunza....Lakini bahati mbaya hali haiko hivyo...Siku zote serikali imekuwa ikisisitiza ongezeko la uandikishaji ama udahili wa wanafunzi huku ikishindwa kuboresha kwa kiwango cha kuridhisha mazingira ya utoaji elimu... Ni lazima ongezeko hili liende sambamba na uboreshaji wa mazingira. ..." Alisema mzazi huyo.

Hata hivyo, Afisa Elimu, Kipenya, alisema kuwa kundi kubwa la wanafunzi wanaosoma katika shule hizo ni la wanafunzi wanaotoka katika familia zenye kipato cha chini ambazo ndio nyingi nchini.

Wanakwenda shule, wanatumia miaka minne bila ya uhakika wowote wa kupata elimu bora. Huku ni kuendelea kutengeneza matabaka katika jamii.

Rahel George ni mwanaharakati mkoani Mtwara, aliuliza kwa nini serikali inashindwa kuboresha mazingira ya shule hizo huku kila mwaka tunaelezwa kuwa bajeti ya elimu inatengewa fungu kubwa la fedha?

Alisema viongozi ni muhimu wakakubali kubadili mienendo ya utendaji wao ili kunusuru taifa hili na kutolea mfano, wa kiongozi mmoja kutumia gari lenye thamani ya zaidi ya Sh milioni 200 ambazo ni kodi za wananchi wanaotaabika kwa kupata huduma mbovu za kijamii ikiwemo elimu.

Aidha Serikali iliwashauri wazazi na wananchi kwa ujumla kuwekeza kwenye elimu ya watoto wao ambapo waliitikia kwa moyo mmoja na kujenga shule wakiwa na matumaini ya kupata mkombozi atakayewasaidia kukabiliana na changamoto za maisha.

Katika mazingira hayo ni muhimu sana kuangalia uwezekano wa kuboresha shule za kata ili kuwawezesha wanafunzi kupata elimu bora ambayo itachangia ukuaji wa uchumi, kukabiliana na changamoto na kusukuma kasi ya maendeleo ya taifa na dunia kwa ujumla



Shule ya sekondari Chuno, Mtwara

# WAZEE MTWARA
# 'Tuna uhuru wa kusema, ila tumo katika anguko'

Na Happy Severine, Mtwara.



Blandina Angalia Mnnari



Stella Chonde

WAKATI hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere anatwaa uhuru wa Tanganyika kutoka kwa wakoloni yaani Waingereza miaka 50 iliyopita alinukuliwa akisema, "Nendeni kwenu baada ya miaka kumi mrudi kuona jinsi tutakavyokuwa tumepiga hatua katika kujiletea maendeleo yetu."

Kwa mara nyingine kipenzi hicho Hayati Baba wa Taifa alinukuliwa akitangaza maadui watatu wa taifa, ambao ni ujinga, maradhi na umaskini, bila shaka Nyerere alidhani kuwa maendeleo ni kitu rahisi kama kumsukuma mlevi.

Leo hii ni miaka 50, Watanzania sasa wanapima utekelezaji wa serikali yao, kimsingi wanajiuliza wapi tumetoka, wapi tulipo na wapi tunakwenda, swali hili ni la msingi kwao ukizingatia ukweli kuwa wengi wa Watanganyika ni wale waliozaliwa baada ya Uhuru.

Mambo yapo mengi ya kujadili na ndiyo maana mwandishi wa makala haya, alizunguka Mjini Mtwara na kufanya mahojiano na baadhi ya wazee ambao walikuwapo wakati wa uhuru, na hapa wanabainisha tulikotoka, tulipo na tunakokwenda.

Bibi Blandina Angalia Mnnari (80) ambaye kwa sasa ni Mwenyekiti wa wazee wa CCM Manispaa ya Mtwara-Mikindani anajibwaga kwenye sofa iliyotengenezwa kwa umahiri mkubwa na kufunikwa kwa kitambaa chenye rangi ya damu ya mzee huku akiwa amevalia sare za CCM.

Anaonekana kuwa ni mwenye uchovu kiasi, kisha ananikaribisha ndani ya sebule na kunisabahi kwa shangwe, kisha ananihoji kusudio la kufika kwangu nyumbani kwake. Nilikuwa mgeni kwani kabla ya hapo sikuwahi kumtembelea bibi huyo ambaye ni nadhifu kwa mavazi hata usafi wa ndani kwake.

Ilinichukua sekunde kadhaa kabla ya kuf[illegible] na macho yang[illegible]eza katika kushangaa mapambo mbalimbali yaliyopo ndani ya sebule hiyo kiasi kilichonifanya nisiamini kwamba Bibi Blandina kuwa ni ajuza, kutokana na unene kiasi nawaza anavyomudu kujituma kutunza mazingira ya nyumba yake.

"Hakuna ubishi kwamba kwa sasa tunaishi tukiwa huru...lakini tupo ndani ya anguko la aina yake.. tunaishi tukiwa na uhuru wa jina tu, hivyo kabla ya kusimama na kuendelea mbele, inabidi kwanza tujue tulipo kwa sasa, tulikotoka na tunakoelekea" anasema Bibi Mnnari.

Anaongeza kuwa: "Tuone pale tulipojikwaa, tusiendelee kulaumu pale tulipoanguka, ni miaka mingi sana mjukuu wangu tangu tupate uhuru... kwa msingi huo mambo pia ni mengi ya kujieleza... yapo mambo ya ujamaa, utii wa serikali na hata masuala ya katiba ya nchi."

Anasema kuwa mara baada ya uhuru taifa lilikuwa limefungamana na sera ya siasa ya ujamaa na kujitegemea hali iliyowafanya Watanganyika waishi kama ndugu moja bila kujali udini wala ukabila, kinyume cha hali ya sasa ambapo ubepari umeliteka taifa na hivyo kuongeza pengo baina ya wenye nacho na wasionacho.

"Azimio la Arusha lilitufanya wote tuwe sawa, tuliishi katika misingi ya kutegemeana, pengo baina ya matajiri na maskini lilikuwa dogo... hali hiyo ilitufariji watu wote, leo hii taifa limepoteza mwelekeo katika hili ndiyo anguko ninalosema... matajiri wanazidi kutunyonya maskini bila ya huruma," anaeleza ajuza huyo aliyeonekana kuhifadhi kumbukumbu nyingi kichwani mwake.

Anasisitiza kuwa hata katika uchaguzi, watu wenye uwezo hata kama hawana uwezo wa kuongoza wanatumia fedha zao kurubuni wanyonge na hatimaye kushika madaraka, kinyume cha hali ya hapo nyuma ambayo uwezo wa mtu kuongoza watu walikuwa wanaupa kipaumbele.

Anaeleza kuwa: "Mbali ya hilo, tumepiga hatua sana katika kutoa uhuru wa mawazo na kuongea, leo hii watu wanakaa na kujadili mambo yasiyowaletea Watanganyika maendeleo ... inafikia hata wakati wanamjadili rais aliyepo madarakani...hapo awali ilikuwa mwiko kwa mtu au kikundi kufanya hivyo, tulikuwa tunasema zidumu fikra za mwenyekiti (Nyerere), katika hili naweza kusema tumepiga hatua."

Anasema kinyume cha sasa, vijana wa enzi hizo walikuwa wanatii maagizo waliyokuwa wanapewa na wakubwa wao... wanajituma kufanya kazi na ndiyo maana taifa lilikuwa halikabiliwi na njaa kiholela, hapakuwa na wimbi la wizi, vibaka kama ilivyo sasa, vijana wa sasa ni wavivu, hawataki kufanya kazi, kila jambo wanataka wafanyiwe na serikali. "Na hali hii naweza kusema mfumo wa viongozi waliokosa uzalendo ndio umesababisha hili."

Aidha Blandina anasema katika kipindi hicho kabla ya uhuru, Watanganyika wengi walikuwa wakitumikishwa na wakoloni bila malipo yoyote yale huku akili na fikra zao zikiwa zimetawaliwa na nidhamu ya woga kwa kufuata amri zilizokuwa zikitolewa na wakoloni.

Hata hivyo, Bibi Blandina anasema kuwa tunapozungumzia mafanikio ya miaka 50 ya uhuru ambao tunatarajia kusherehekea hapo Desemba 9 mwaka huu , ni mambo mengi sana yamefanyika katika serikali inayoongozwa na CCM.

Akielezea mafanikio yaliyofanyika toka kupatikana kwa uhuru wa Watanganyika, Blandina anasema kuwa kwa mikoa ya kusini yaani Lindi, Mtwara na Ruvuma imefanikiwa kupata mafanikio mengi sana katika upande wa elimu, miundombinu ya barabara, maji, umeme na huduma za afya mafanikio hayo hayakuwepo hapo awali.

Blandina anasema mbali na kuwepo mafanikio hayo, bado hatuwezi tukajivuna na kusema tumepiga hatua mbele endapo hayo mafanikio yote hayatolewi vizuri kwa Watanganyika.

"Hivi mjukuu wangu unapozungumzia mafanikio unamaanisha nini...ngoja nikueleze maana naona wewe bado mtoto mdogo...hatuwezi tukasema tuna mafanikio wakati shule zilizojengwa kwa wingi hazina walimu na vitendea kazi vya kutosha...wakati huo huo huduma zitolewazo hospitalini haziridhishi," anasema Bibi Blandina.

Anaongeza kuwa, tunataka mafanikio yaliyokamilika. Anafananisha na enzi za Waingereza kuwa shule, zahanati na maduka vilikuwa vichache, lakini vyote hivyo vilikuwa vinajitosheleza ndiyo maana anahoji "Utasemaje tumepiga hatua kuwa na majengo yasiyoleta maendeleo kwa wananchi?".

## SELEMANI MBULLU (75): SIJAONA KITU

Selemani Mbullu (75) mkazi wa manispaa ya Mtwara-Mikindani naye hakusita kueleza kile anachokifahamu ndani ya miaka 50 ya uhuru, akiwa nje ya nyumba yake ambayo bado haijamalizika, mzee huyo hakusita kubainisha kutokana na ugumu wa maisha unaomkabili. Kwa sasa yeye haoni kama kumekuwapo na hatua zozote za kimaendeleo tangu kupatikana kwa uhuru.

"Kwangu sioni hatua yoyote ya mafanikio mbali ya hali kuzidi kuwa mbaya kimaisha, wakati tunapata uhuru fedha ilikuwa ngumu kuipata, lakini ilikuwa na thamani na hivyo hali ya maisha ilikuwa rahisi, leo hii fedha haipatikani na maisha n[illegible] magumu...yako wapi matunda y[illegible] uhuru?" anauliza Mbullu.

Anafafanua kuwa: "M[illegible]nda ya uhuru wanaofaidi ni wachache, wengi tunaishi huku tukiwa tumepoteza matumaini ya maisha bora, leo tunaadhimisha miaka 50 ya uhuru huku kundi la matajiri likizidi kuwanyonya maskini."

Kwake anasema: "Kujenga barabara, zahanati, shule, huduma zamaji na umeme ni wajibu wa serikali, sasa we ulitaka serikali ifanye kazi gani, miaka 50, huduma mbovu za matibabu, elimu halafu unasema kuna maendeleo, mimi nasema hakuna maendeleo yaliyofikiwa."

Kwa mujibu wa Mbullu, umri wa nchi tangu kupata uhuru ni mkubwa kuliko jitihada zilizofanywa katika kupambana na maadui maradhi, ujinga, umaskini na rushwa.

"Unapozungumzia miaka 50 ya uhuru...lazima tuangalie jitihada zilizofanywa katika kupambana na maadui watatu, maradhi, ujinga na umaskini, ni dhahiri kuwa bado jitihada si za kuridhisha kwa kipindi chote hiki cha miaka 50 ya uhuru...huduma bado ni mbovu na tabaka kati ya matajiri na maskini ni kubwa mno," anasema Mbullu kwa kujiamini.

## STELLA CHONDE (65): NAWASHANGAA WASIOONA MAENDELEO MAKUBWA

Bibi Stella Chonde (65) yeye anapingana na mtazamo wa Mzee Mbullu kwa kile alichokiita kuwa ni hatua kubwa ya maendeleo iliyopigwa na taifa katika kipindi cha miaka 50 ya uhuru.

"Ninawashangaa sana wale wanaosema hakuna mafanikio, angalia hapo awali usafiri ulikuwa wa shida, tulikuwa tunatembea kilomita 10 hadi 20 kwa miguu, leo hii tunasafiri kwa dakika chache. Kwa mtazamo wangu yapo mambo tumepiga hatua na yapo mambo tunatakiwa kuweka mkazo," anasema Bibi Chonde.

Anasema: "Sisi wa mikoa ya kusini tunayo kila sababu ya kufurahia miaka 50 ya uhuru kwa mafanikio ukizingatia hali ya barabara kutoka Mtwara, Lindi kwenda Dare s Salaam, ilikuwa inatuchukua wiki mbili kwenda Dar wakati wa masika...leo hii siku moja tu, haya ni mafanikio makubwa."

Ukiachilia mbali suala la barabara, Bibi Chonde anasema kumekuwepo na ongezeko kubwa la upatikanaji wa huduma za kijamii, ongezeko la zahanati na hospitali za wilaya, maji, umeme na mengi ambayo bila kuyataja yanaonekana machoni mwa watu tofauti na hapo awali kabla ya uhuru.

Bibi Chonde anasema mbali na jitihada zote hizo za kuifanya Tanganyika ya maendeleo ndani ya miaka 50, Watanganyika ambao kwa sasa ni Watanzania hawana budi kuondoa tabaka lililojengeka baina ya matajiri na maskini.

Aidha anasema, ingawa kwa sasa wananchi wamepoteza uaminifu kwa viongozi wao kwa kukosa uzalendo wa nchi yao, aliomba serikali irudishe mfumo wa vijana kwenda Jeshi la kujenga taifa (JKT) ili kurudisha heshima na uzalendo wa nchi kama ilivyokuwa hapo awali enzi za Mwalimu Nyerere.